



***Njia (route) ya mkonga katika kisiwa cha Pemba***

**Mafanikio na shughuli zinazoendelea toka kuanzishwa kwa ZICTIA:**

1. Kuunganishwa na mkonga wa mawasiliano kwa Taasisi za Serikali zaidi ya 140 kwa matumizi ya huduma mbali mbali za kimtandao.
2. Kuanza kwa matumizi ya mkonga wa baharini Fumba – Dar es salaam na Tanga – Pemba na upo tayari kwa ajili ya kupitisha mawasiliano (traffic) ya wateja baina ya sehemu hizo
3. Kueneza elimu ya uhifadhi taarifa (data storage) kwa Taasisi za Serikali .
4. Kushuka kwa gharama za mtandao Zanzibar inayosababishwa na kuwepo kwa Mkonga kutoka Zanzibar kwenda Dar es salaam.




***Mkonga unaotumika kusafirishia taarifa***

**WASILIANA NASI;**
**Simu :** 024 2235784
**Barua Pepe :** info@zictia.go.tz
**Tovuti :** www.zictia.go.tz
**S.L.P 1823,**
**Mazizini, Zanzibar.**

ZICTIA

## WAKALA WA MIUNDOMBINU YA TEHAMA ZANZIBAR

***"Kwa pamoja tuilinde miundombinu ya TEHAMA ili kuimarisha mawasiliano na uchumi wa Zanzibar"***




***Njia (route) ya mkonga katika kisiwa cha Unguja***

## A. HISTORIA KWA UFUPI

Wakala wa Miundombinu ya Tehama ya Zanzibar ni Taasisi ya Serikali inayosimamia mkonga wa mawasiliano pamoja na kituo cha kuhifadhia taarifa (Data Center) ambayo Ilianzishwa rasmi tarehe 4 Disemba 2018. Wakala inahusika na miundombinu yote ya teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

**Dira:**

- Kuboresha miundombinu ya Tehama ya Zanzibar itakayosaidia kukusanya mapato kwa lengo la kukuza uchumi wa Zanzibar.

**Dhamira:**

- Kuhakikisha Wizara, Mashirika na Taasisi zote za Serikali, zinaunganishwa na kutumia huduma zinazopatikana kupitia mkonga wa Taifa, hii itasaidia upatikanaji wa haraka kwa huduma za kijamii zinazotokana na mkonga wa Taifa.
- Kutoa nafasi kwa vyombo na Taasisi binafsi kujiunga na huduma ya Mkonga, hii itasaidia katika kukuza teknolojia ya mawasiliano kwa haraka na kiurahisi zaidi.
- Kukitumia kituo kikuu cha kuhifadhia taarifa (Data center) ili kuhakikisha usalama wa taarifa na mifumo.

## B. KAZI NA MAJUKUMU YA ZICTIA

- Kusimamia na kuendeleza miundombinu ya teknolojia ya habari na mawasiliano na huduma zake.
- Kusimamia na kuendeleza kituo kikuu cha kuhifadhia taarifa **"Data Center"** Zanzibar .
- Kusimamia na kuendeleza anuani mtandao **"IP address"** Zanzibar.
- Kuimarisha usalama, ulinzi, uchumi na maendeleo ya miundombinu ya teknolojia ya habari na mawasiliano kibiashara.
- Kutoa muongozo wa miundombinu ya TEHAMA Zanzibar.
- Kupanga na kuendeleza miundombinu ya TEHAMA Zanzibar.
- Kutoa ruhusa ya matumizi ya miundombinu ya TEHAMA kwa kampuni zote zinazotoa huduma ya mawasiliano ya simu na watoa huduma za TEHAMA Zanzibar.
- Kutoa huduma ya kuunganisha kupitia miundombinu ya TEHAMA kwa taasisi zote za Serikali Zanzibar.
- Kutoa huduma zitokanazo na miundombinu ya TEHAMA.
- Kutoa elimu kwa umma ili kukuza uelewa na upashaji wa taarifa kwa umma kuhusu unyeti wa miundombinu ya TEHAMA.

## C. HUDUMA ZITOLEWAZO NA ZICTIA

Wakala wa Miundombinu ya Serikali kwa sasa inatoa huduma zifuatazo;

- Huduma ya Uwekaji wa vifaa vya elektroniki katika Miundombinu yetu kwa kitaalamu inajulikana kama **"Colocation".**

- Huduma ya Ukodishaji wa seva kwa ajili ya uhifadhi wa taarifa au mifumo ambayo kitaalamu inajulikana **"Virtual Mashine"** . Huduma hii humuwezesha Mteja na Taasisi za Serikali kupatiwa sehemu ya seva zetu kulingana na mahitaji yao ili kuhifadhi taarifa zao na mifumo katika kituo kikuu cha kuhifadhia taarifa (Data Center) chenye kuzingatia usalama, unafuu, uendelevu na jumuishi. Huduma hii humsaidia mteja huokoa gharama za kununua seva nzima pamoja na gharama za uendeshaji wa kifaa hicho.



***Miongoni mwa miundombinu katika kituo kikuu cha kuhifadhia taarifa (Data center)***

- Huduma ya kuunganishwa kwa Taasisi za serikali na wateja wa taasisi binafsi na mkonga wa Taifa wa mawasiliano kwa ajili ya huduma ya mitandao ya **"internet"** na **"intranet"** yenye kasi kulingana na Mahitaji ya Mteja.

- Huduma ya kukodisha uwezo wa kupitisha mawasiliano / taarifa **"traffic"** kwa kitaalamu **"capacity leasing"** kwa Dar es salaam –Fumba na Tanga – Pemba.

- Huduma ya Kupitisha taarifa katika mtandao binafsi uliopo ndani ya miundombinu yetu **"VPN"** Huduma hii huwezesha kuimarisha usalama wa mawasiliano, taarifa na mfumo wa mteja.

- Huduma ya IP MPLS.

## D. MALENGO NA MPANGO MKAKATI

ZICTIA imejiwekea malengo na mpango mkakati kama ifuatavyo ;

- Kutoa huduma za miundombinu ya TEHAMA yenye unafuu, uendelevu, usalama na jumuishi yenye kuwezesha kutoa huduma kwa umma .

- Kuimarisha na kuendeleza Miundombinu ya TEHAMA na huduma zake.

- Kushajihisha na kuimarisha mchango wa miundombinu ya TEHAMA kwa maendeleo ya uchumi Zanzibar.

- Kufanya tathmini ya kijamii na mazingira kwa ajili ya kuhifadhi na kupata ufumbuzi wa athari zinazoweza kutokea katika miundombinu ya TEHAMA kwa umma.

- Uvumbuzi na upanuzi wa huduma zitokanazo na miundombinu ya teknolojia ya habari na mawasiliano kadri ya uhitaji wa huduma husika kwa umma.

- Kuhakikisha Taasisi za Serikali zinaunganishwa na mkonga wa mawasiliano ili kurahisisha na kuboresha upatikanaji wa huduma za mawasiliano na kuokoa gharama kubwa ambazo zilikuwa ni mzigo kwa serikali.




***Mkurugenzi wa ZICTIA Eng. Shukuru A. Suleiman (kushoto) , na Mkurugenzi wa TTCL Nd. Waziri Kindamba (Kulia) wakikabidhiana mkataba wa huduma za matumizi ya Mkonga wa Mawasiliano ambayo ZICTIA inaiuzia huduma hio TTCL.***